



Lau kama ningekuwa na dhahabu kubwa mfano wa mlima Uhudi, basi ningependa zisipite siku tatu nikiwa namiliki chochote katika mali hiyo zaidi ya kile ninachokihifadhi kwaajili ya kulipa madeni

Kutoka kwa Abuu Huraira -Radhi za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake- kutoka kwa Mtume - Rehema na Amani ziwe juu yake-Amesema: "Lau kama ningekuwa na dhahabu kubwa mfano wa mlima Uhudi, basi ningependa zisipite siku tatu nikiwa namiliki chochote katika mali hiyo zaidi ya kile ninachokihifadhi kwaajili ya kulipa madeni".

[Sahih] [Imepokelewa na Al-Bukhaariy na Muslim na tamko ni la Bukhaariy]

Lau kama ningekuwa ninamiliki katika mali kiasi cha dhahabu halisi kama mlima Uhudi, basi ningekitoa chote katika njia ya Mwenyezi Mungu, na nisingebakisha katika mali hiyo ila kiasi ninachokihitaji kwa kukidhi mahitaji, na kulipa madeni ninayodaiwa.

<https://sunnah.global/hadeeth/sw/show/3850>

